

## Kiswahili na Maendeleo Mashambani Nchini Kenya

Makoti Vifu Saidi

*Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Machakos*

*E-mail: [vifusaidi@gmail.com](mailto:vifusaidi@gmail.com)*

### IKISIRI

*Makala hii itatathmini umuhimu wa lugha (Kiswahili) katika kuchangia maendeleo nchini Kenya. Maendeleo yamejelezwa na wataalamu mbalimbali. Chambers (1997) ameleeza ‘maendeleo’ kwa usahili kabisa kuwa ni ‘mabadiliko mazuri’ (nchini au duniani). Alan Thomas (2000) ameyaeleza kama kuboreka kwa hali ya maisha, afya na maisha bora kwa wote na mafanikio ambayo huleta uzuri wa maisha kwa jamii yote. Haya hutokea kwa awamu ya muda mrefu. Maendeleo kwa jumla humaanisha mabadiliko chanya ya mwanadamu katika harakati zake zote za kimaisha. Maendeleo ni lazima kwa mwanadamu duniani. Hakuna wanadamu wanaobaki kama walivyo miaka nenda miaka rudi. Kuna maendeleo ya kibinagsi na ya kijamii. Yote haya huwezeshw na kiwango cha uchumi. Uchumi hukua kutokana na uzalishaji mali. Uzalishaji mali hutokea katika mashamba na mitambo au viwanda. Uwezo huu huletwa na jamii kujifunza mbinu na stadi za uzalishaji mali. Mtu anapojifunza stadi fulani, lazima atumie lugha, lugha anayowielewa. Kwa hivyo, stadi haziletwi na Kiingereza bali lugha yoyote ile. Nchi nyingi ulimwenguni hazitumii Kiingereza na zimeendelea sana, mfanu Ujarumani, Ufaransa, Italy, Malasyia, Korea Kisini na kadhalika. Kwa hivyo, natujiulize, je, hapa Kenya tunaweza kutumia Kiswahili kujifunza mbinu na stadi mbali mbali za kuzalisha mali? Hii ni kwa sababu Kiswahili ni somo la lazima nchini kutoka shule za msingi hadi shule za sekondari. Aidha ni lugha rasmi na ya taifa. Hivyo ni lingua franca nchini. Katika makala hii ninajaribu kudadisi swala hili na kutoa mifano kadhaa iliyopatikana nchini Kenya.*

**Maneno makuu:** maendeleo, uchumi, mawasiliano, lugha, elimu

### UTANGULIZI

Maendeleo ni muhimu sana kwa nchi yoyote ile ili yamfaidi mwananchi. Maendeleo huathiri mwananchi kwa kiwango kikubwa na moja kwa moja. Nchi ikiwa na maendeleo duni, mwananchi hana budi kuwa na maisha duni pia, na nchi ikiwa na maemdeleo bora, mwananchi naye atakuwa na maendeleo na maisha bora vile vile. Ili nchi kupiga hatua kimaendeleo, inahitaji sera za serikali kufahamika na kueleweka barabara na wananchi wote nchini na kuungwa mkono. Mifano mizuri ni nchi za Asia ya Mbali; Korea Kusini, Malaysia, Indonesia, Thailand n.k na nchi za Ulaya. Hizi ni nchi ambazo zinatumia lugha zao asilia katika mawasiliano yao ya aina yoyote ile ikiwamo mafunzo shulen na vyuoni. Hivyo, hapa Kenya, lugha ya kuelezea sera za serikali na mikakati ya maendeleo, lazima iwe lugha inayotumiwa na wote, wawe waliosoma au la. Lugha hiyo si nyingine ila Kiswahili, ambayo inatambuliwa kikatiba kama lugha rasmi na ya kitaifa (*Katiba ya Kenya*, 2010). Lakini natujiulize, je, Kiswahili kinatumika ipasavyo katika kueleza na kuendeleza sera za serikali hata wakaazi wa mashambani waelewe sera hizo? Vile vile kinatumika kuwafunza watu stadi na mbinu mbalimbali ili kuboresha uzalishaji mali? Haya ni masuala ambayo tutayadadisi katika makala hii na kuyafumbua. Nitatoa mifano kutoka hapa nchini Kenya na kwengineko ulimwenguni kudhihirisha kuwa lugha asili inapotumika katika mafundisho na usambazaji wa sera

za serikali, maendeleo hupatikana.

*Dhana ya Maendeleo*

Kabla ya kudadisi na kutathmini swala la Kiswahili na maendeleo, nitajaribu kufafanua maendeleo ni nini.

Maendeleo ni mchakato mseto wa kadri unaojumuisha upangaji mpya wa mifumo yote ya kiuchumi na kijamii. Lazima maendeleo yajumuishe mabadiliko ya miundo mbinu, msimamo, na asasi pia, kukua kwa uchumi, kupunguka kwa ukosefu wa usawa na kumaliza umasikini katika jamii (Todaro, 1992). Hivyo ni kwamba, maendeleo ya nchi nyingi si kuongezeka kwa mapato ya nchi tu.

Maendeleo inamaanisha si ukuaji wa uchumi tu lakini pia ni kuboresha hali ya maisha ya umma, kujumuika katika uchumi ambao ni tajiri kimuundo na kiteknolojia, na ujenzi wa uchumi ambao una muundo wa kudhibiti ukuaji na kuzidi kuwa bora (Murdoch, 1980).

Roodney (1989:29) anadai kwamba maendeleo katika jamii ni mchakato wenyewe mawanda mapana. Katika kiwango cha mtu binafsi, yanamaanisha kuwa na stadi na uwezo zaidi, uhuru zaidi, ubunifu, nidhamu, uwajibikaji na uwezo wa kuwa na bidhaa tofauti tofauti. Tunaporejelea maelezo haya, mtu anatakikana kuwa na stadi zaidi zinazozaa uwezo wa kiuchumi. Stadi hizi mtu hufunzwa kwa lugha anayoielewa. Kwa hivyo hapa Kenya tukihitaji watu wawe na stadi zaidi, basi wawe watajifunza kwa Kiswahili ili wengi wafaidi. Hii ni kwa sababu, Kiingereza hakifahamiki na watu wengi kama Kiswahili. Tunapofanya hivyo, tunamuwezesha mtu binafsi na kutumia stadi hizi kwa maendeleo yake binafsi na nchi kwa jumla. Maendeleo ya kiuchumi huletwala na uzalishaji mali bora na nyingi. Hili hufikiwa katika nchi iwapo wafanyakazi watakuwa na stadi bora zinazoweza kuzalisha bidhaa bora. Stadi hizi hupatikana kupidia mafunzo shulenii au viwandani.

Kwa hivyo 'maendeleo' ni dhana pana ambayo inajumuisha maisha yote ya mwanadamu na kwamba lengo liwe kuyaboresha. Kama wadaivyo Todaro (1992) na Desai (1982), nchi itakuwa haijaendelea ikiwa kiwango cha uchumi kitakuwa kimekua kwa asilimia maridhawa lakini wengi nchini bado ni masikini na wanakosa miundo mbinu ya kimsingi. Yaani, bado wengi hawana kazi, wafanyakazi hawana stadi, wananchi hawapati huduma bora za matibabu, hawana umeme, hawana maji safi n.k. Hivyo, jukumu la serikali yoyote ile ni kuleta maendeleo nchini, na lazima miundo mbinu hii itiliwe maanani na serikali ijaribu kupiga vita umaskini, ukosefu wa kazi, magonjwa n.k. Hii itafanya umma wote uendelee kwa jumla. Iwapo utajiri utakuwa chini ya watu wachache nchini, basi nchi itazidi kukosa maendeleo na kubaki maskini.

Katika makala hii ninachukulia dhana "maendeleo" kama ilivyoelezwa hapo juu na Todaro, Desai na Roodney. Ili kuwa na maendeleo nchini, kuna mambo kadhaa ambayo lazima yatimizwe:

i) Lazima habari zisambazwe kwa umma juu ya sera na mikakati ya serikali, na kutoa ushauri kwa umma jinsi ya kujiendeleza.

ii) Lazima udundulizaji na utunzaji wa rasilimali, elimu na mafunzo yafanyike ili umma umudu kuendelea na kutumia stadi zao, uwezo na tafakuri.

iii) Ni kuwepo kwa asasi faafu za kijamii, kiuchumi na kisiasa ambazo zinawezesha na kuruhusu

ukuaji wa stadi hizo za uwezo wa kuongeza uzalishaji mali (Murdoch, 1980:170-171).

La msingi hapa ni umma ufahamishwe, upate stadi na kuwa huru kuweza kutumia uwezo wake kuzalisha mali zaidi. Mambo haya yatafikiwa kwa kuhamasisha na kufunza umma stadi mbalimbali katika uzalishaji mali. Yote hawa hutimizwa kwa kuititia mawasiliano. Mawasiliano hutimia kwa mpewa ujumbe anapoelewa ujumbe huo kutoka kwa mtuma ujumbe. Katika mawasiliano lazima lugha itumike, inayofahamika kwa pande zote mbili, mtuma na mpokeaji ujumbe (Mbithi, 1974). Hapa nchini Kenya mawasiliano kama haya yanawezekana kwa kuititia lugha ya Kiswahili kwani ndiyo lugha inayofahamika kwa wengi kuliko lugha yoyote ile. Kiswahili ni *lingua franca* Afrika Mashariki kote (Chimera, 1998). Kiswahili ni lugha ya Taifa na rasmi nchini Kenya (Katiba ya Kenya, 2010).

Watu wengi nchini Kenya wanaishi mashambani na lugha ifahamikayo zaidi kando na lugha ya kwanza ni Kiswahili. Kuititia Kiswahili, mawasiliano yatawafikia watu wengi zaidi nchini Kenya. Mashambani, kazi muhimu ni ukulima na mijini ni viwanda. Huko mashambani, ili wananchi wamudu kukuza chakula zaidi, wanahitaji mbinu mpya za kisayansi. Mbinu hizi zimo vitabuni kwa lugha za kigeni mfano Kiingereza hapa nchini Kenya. Lugha hii ni ya watu wachache. Kwa hivyo, kuelewa mbinu hizi vyema, lazima mafunzo yaye kwa Kiswahili, lugha wanayoifahamu vyema wakulima. Au lugha za kwanza, iwapo mtaalamu anafahamu lugha ya kwanza ya wakulima. Maofisa wa Kilimo wanatoka katika jamii mbalimbali, na kufanya kazi katika Kaunti mbali na zao na lugha ya kwanza ni tofauti na zao (si wakati wote). Kwa hivyo chaguo ni lugha ya Kiswahili kwa mawasiliano.

Murdoch (1980), Desai (1982), Miller (1988), Todaro (1992), wote wanakubaliana kuwa ukulima ndio umechangia pakubwa katika nchi nyingi ulimwenguni kuleta maendeleo ya kiuchumi. Umuhimu wa ukulima ni ule mchango wake katika kuinua hali ya maisha kifedha. Kwa hivyo, mchango wa kwanza kabisa wa kilimo ni kuinua hali ya maisha ya umma mashambani (Murdoch, 1980:172). Murdoch anaendelea kudai kuwa uchumi bora wa nchi kama vile Ulaya, Marekani na Japoni katika karne za 18, 19 na 20 ulichangiwa pakubwa na kilimo (Kama hapo juu:183).

Mnamo 1880, wakulima huko Japoni walionyesha uwezo wao kwa kukubali mbinu mpya za ukulima, na wale waliopata ujuzi zaidi mashambani, walitumiwa kama walimu kufundisha wenzao katika vyuo vya kilimo na pia kuwa washauri nyanjani kwa kutumia Kijapani. (Kama hapo juu:187). Huko India, Taiwan, Korea Kusini, mambo yalikuwa vivyo hivyo (Desai, 1982; Todaro, 1992). Lugha za mawasiliano zilikuwa lugha zao asili au za kwanza. Je, kwa nini nchini Kenya jambo hili lisifanyike na lugha ipo ya Kiswahili ambayo ni *lingua franca* nchini?

#### *Uwezekano wa Kiswahili kutumika kufundishia Umma Maswala ya Maendeleo*

Tangu Tume ya MacKay (1984) juu ya Chuo Kikuu cha Pili hapa Kenya kuitisha Kiswahili kuwa somo la kutahiniwa katika shule za msingi na sekondari, watu wengi sana hapa Kenya wamesoma Kiswahili na kuifahamu lugha hiyo. Sasa ni miaka takribani thalathini na tatu (33) kwa Kiswahili kuwa somo la lazima nchini Kenya. Kwa hivyo, wazungumzaji ni wengi sana nchini na Kiswahili kinafahamika katika pembe zote za nchi. Jitihada ni zifanywe kukitumia kufundishia watu

mashambani stadi mbalimbali kama vile za ukulima, uashi, useremala, uhunzi n.k. Jambo hili likifanyika, Wakenya watapata ujuzi wa kiufundi na wa kilimo. Hili litasaidia kuzalisha mali zaidi na bora, ambazo zitauzwa nchini na hata nchi za nje kupata fedha za kigeni na kuendeleza uchumi wa Kenya.

Wataalamu wa mitalaa wanafaa wakumbatie wazo hili na kugeuza njia ya kufundishia hususan masomo ya kiufundi. Istilahi zitajitokeza tu. Hoja hii inashadidiwa na Fromkin, Rodman na Hymns (2007:88-89) wanaposema kuwa kunapotokea pengo la kileksia (*lexical gap*), wazungumzaji watazua istilahi za kujaza pengo hilo na zitatumika katika mawasiliano ingawaje si sanifu, na huenda zisiwepo katika makamusi wakti huo. Vile vile wakatoa mifano ya jinsi Kiingereza kilivyoza maneno mapya kujaza pengo hilo; *unsystem, uglification, Chomsykayan, breathable, chopoffable* n.k. Na maneno haya yanatumika katika mawasiliano ingawaje si sanifu. Hatuwezi kupata istilahi bila kuanza sera hii. Ikumbukwe safari ni hatua. Kwa mfano, kwa mujibu wa Rashid (1992: 194-195), lugha ya Dari (Persian) huko Afaghastan, imezaa istilahi za kiufundi, mifano: *enjiniri* (engineering), *motirsikel* (motorcycle), *partaim*(part-time). Wenzetu hawa wanatumia lugha ya Dari katika kufundisha uhandisi Chuo Kikuu. Hivyo hapa Kenya, jambo hili linawezekana kwa kutumia Kiswahili. Kwa mfano, ugonjwa wa HIV/AIDS ulipoingia Afrika Mashariki, istilahi zilipatikana kwa dhana zinazohusishwa na ugonjwa huu, mfano *UKIMWI* (HIV/AIDS), *unyanyapaa* (stigma), *virusi* (virus), n.k. Kwa sasa hivi istilahi nyingi zimezaliwa kusimamia dhana mbalimbali, mfano *nywinywila* (password), *tarakilishi* (computer), *kipakatalishi* au *kiuweo* (laptop), *uwajibikaji* (accountability), *uwazi* (transparent) n.k. La msingi ni Kiswahili kitumike katika kueneza sera za serikali na kutoa stadi kwa vijana ili kuzalisha mali na kuchipua maendeleo mashambani. Wazungumzaji wa Kiswahili watazalisha istilahi kukamilisha mawasiliano yao.

Tuangalie mifano michache ifuatayo kutokana na utafiti huu juu ya Kiswahili kutumika mashambani na katika viwanda vya Jua Kali vya ufundi.

#### *Mifano Nchini Kenya*

Tatizo kubwa nchini Kenya ni kupuuza Kiswahili katika maswala muhimu ya nchi. Tutakapozingatia kwa dhati mawasiliano yetu kwa lugha ya Kiswahili, istilahi zitapatikana. Mfano mzuri wa kutumia Kiswahili mashambani katika miradi ya kiuchumi ni huko tarafa ya Njoro katika Kaanti ya Nakuru. Rono (2001:137) anaeleza kuwa wakulima wanawake kwa wanaume waliopata elimu kwa kuititia lugha za Kiswahili na Kiingereza, waliweza kuongeza uzalishaji mali maradufu kwa sababu ya mawasiliano bora katika mawazo na uvumbuzi wa mbinu mpya za ukulima. Mawasiliano haya yalikuwa mwafaka kwa sababu Kiswahili kilitumika pamoja na Kiingereza kati ya wakulima hao na wataalamu nyanjani. Wanapozalisha mali zaidi biashara nayo hupanuka, wapate fedha zaidi na kuongeza maendeleo.

#### *Kaanti ya Kwale*

Huko Kaanti ya Kwale, tarafa ya Matuga, Lokeseni ya Golini, kikundi cha akina mama cha 'Jitahidi' cha ufugaji ng'ombe wa maziwa, niliwahoji kuhusu utaalamu wanaoutumi wa kudunga ng'ombe sindano, kupuliza dawa za kupe waliupata wapi. Walinielezea kuwa walifundishwa na Ofisa wa Wanyama wa nyanjani kwa lugha ya Kiswahili. Akina mama hawa hawajui kusoma wala

kuandika na wanadunga ng'ombe wao sindano wanapokuwa wagonjwa au kuzuulia magonjwa. Kiingereza hakikutumika hapo, na shughuli za ufugaji zinaenda vyema. Wanapata maziwa na kuza. Mweka hazina wao aliniarifu kuwa hupata takriban shilingi elfu kumi na mbili kwa mwezi kutoka ng'ombe wao wawili.

Katika eneo hilo hilo, mfugaji mwingine wa ng'ombe za kienyeji, Mzee Salimu Mohamed Madindima mwenye umri wa miaka sabini hivi (70), hajui kusoma wala kuandika lakini huwatibu ng'ombe wake kwa kuwapa dawa na kuadunga anapogundua ni wagonjwa. Mtafiti alishuhudia kitendo hiki (Agosti 25, 2014) alipomtembelea nyumbani kwake. Alipomuhoji anawezaje kutimiza huduma hii na hajui kusoma. Alinifahamisha alifunzwa haya yote na Daktari wa Mifugo wa nyanjani. Alifunzwa dalili za magonjwa mbalimbali na dawa za kutibu magonjwa hayo. Alifundishwa vipimo mbalimbali vya matumizi ya dawa za kutibu mifugo. Huadunga ng'ombe wake na kuwatibu. Nilipomuuliza alifundishwa kwa lugha gani, alinieleza Daktari alitumia Kiswahili. Kwa sasa hivi hahitaji daktari. Yeye mwenyewe huenda duka la madawa akanunua dawa na kuwatibu ng'ombe wake.

#### *Kaunti ya Uasin Gishu*

Katika Kaunti ya Uasin Gishu, mtafiti alizuru kiwanda kimoja cha jua kali mjini Eldoret. Hapo alimkuta fundi wa kutengeneza mitambo ya kusaga mahindi inayotumia umeme, Bw. Allan Onyango (umri wa miaka 45) na wanafunzi wake. Nilimuhoji kiwango chake cha masomo, akaniambia ni darasa la saba. Nikamuuliza jinsi alivyopata ujuzi huo. Akaniarifu alijifunza katika kiwanda cha jua kali huko Kaunti ya Kisumu. Akaniarifu alifundishwa kwa kutumia Kiswahili, na majina ya vifaa alivyovitumia mwalimu wake alivitaja kwa majina ya Kingereza wakati wa mafunzo. Na kwa sasa hivi hutengeneza mitambo minne kwa wiki akiwa na wanafunzi wake. Wanajifunza hapo kwake, huwafunza kwa lugha ya Kiswahili. Kuna majina kama *motor, grinder, switch*, msumeno wa umeme, vyuma n.k hutumia matamshi ya Kiswahili kwa kuvirejelea vifaa hivyo.

Vile vile mtafiti alizuru gereji ya Jua Kali katika eneo la Asis Hoteli mjini Eldoret na kuwahoji mafundi wa magari wakiwemo wanafunzi katika gereji hizo. Alisikia Kiswahili kikitumika katika harakati zote. Vifaa mbalimbali viliitwa majina yao ya Kiingereza lakini kwa matamshi ya Kiswahili mfano *ekzosti, tairi, handibreki, jeki, nati, indiketa* n.k. Baadhi ya vifaa vilipewa majina ya Kiswahili mfano '*strainer*' katika *oil sump* walikiita '*kichungi cha sampu*', '*filter*' walitumia neno '*kichungi*'. Na kazi iliendelea vyema magari yakinengenezwa bila kikwazo cha mawasiliano.

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba Kiswahili kinaweza kutumika mashambani kuelimisha na kufunza stadi mbalimbali ili kuchangia maendeleo ya mtu binafsi, umma na nchi kwa jumla. Istilahi mbalimbali zitapatikana pindi tutakapoanza kukitumia Kiswahili kama njia ya kufundishia shuleni na vyuoni. Kuna njia mbalimbali za uzalishaji wa msamiati. Njia hizi zikitumika, msamiati utazalishwa kuititia utaalamu huu wa leksigrofia.

#### *Kaunti ya Machakos*

Mtaa wa Grogan, Machakos ni eneo la viwanda vya Jua Kali. Ingawaje viwanda hivi ni ithibati ya kutoendelea, lakini serikali ikisaidia mafundi hawa, kutazaliwa eneo la viwanda vya hali ya juu.

Nchi za Korea Kusini na Uchina zilianza kuwa nchi za viwanda kama zijulikanazo leo, kwa kupitia viwanda vya Jua Kali. Serikali za nchi hizi ziliwekeza katika viwanda hivi na mafundi kupewa mafunzo ya hali ya juu kwa kutumia lugha zao asili. Mtaa huu wa Grogan una mafundi wengi; wa magari, wa viti vya magari, uchomeleaji, wahanzi, seremala n.k. Mtafiti alizuru eneo hili na kuteuwa kimakusudi mafundi wawili; mmoja wa umeme wa magari (*motor wiring*) na mmoja wa uchomeleaji (*welding*). Fundi wa umeme wa magari anaitwa Bw. Stephen Mumo mwenye umri wa miaka arubaini na tano (45) mzaliwa wa Mtituni, Machakos. Alinielezea kuwa alisoma hadi darasa la nane (STD. 8). Hakuendelea kwa upungufu wa pesa kwani baba yake alikuwa masikini. Akajiunga na mafundi wa Jua Kali hapa Grogan. Sasa hivi ndiye fundi msika katika eneo hili kama fundi wa umeme wa gari. (Ameshawahi kurekebisha gari la Mtafiti huyu.)

Nilipomuhoji alijifunza ufundi huo kwa lugha gani, alijibu kwamba alijifunza kwa Kikamba na Kiswahili. Kiingereza kilitumika kutaja vifaa au vipuri vya magari vya umeme mfano *alternator, distributor, socket* n.k. Alijivunia ujuzi wake na akanieleza kwamba hata wanafunzi wa Diploma walio waandamizi nyanjani (*attachment*) huwafundisha ilhali hana cheti chochote cha kusomea ufundi huo.

Fundi wa pili ni Bw. Safari Mbithi mwenye umri wa miaka hamsini na tatu (53), mzawa wa milimani, Machakos. Alisoma hadi darasa la nne (STD 4). Akaacha shule akajiunga na mafundi wa Grogan kujifunza uchomeaji. Lugha alizozitumia kujifunza, aliniarifu ni Kikamba na Kiswahili. (Alimchomea Mtafiti huyu bomba la kutoa moshi (*exhaust pipe*) la gari yake mwaka wa 2016 hadi leo 2018, halijaleta matatizo.) Mtafiti alimfumania akitengeneza jiko la kuoka keki wakati wa utafiti huu. Jiko hilo alilikamilisha na akadai ni agizo la mwokaji na ameshatengeneza mengi yanayotumika hapa mjini Machakos.

Mifano hii miwili, ni dhihirisho kwamba lugha yoyote inaweza kutumika katika kufundishia ujuzi wowote. Kwa hivyo Kiswahili kama *lingua franca*, lugha rasmi na lugha ya taifa hapa Kenya (Chimera, 1998; Katiba ya Kenya 2010) kinaweza kutumika, kufundishia ujuzi mbalimbali na kuwawezesha vijana kuzalisha mali na kujiajiri ili kuleta maendeleo hapa nchini Kenya. Ufundu hauhitaji Kiingereza bali lugha yoyote ile inayoeleweka na kuwasilisha ujumbe katika jamii.

### **Njia za Kuzalisha Msamiati katika Lugha**

Wanaleksigrofia hutumia njia kadhaa kuzalisha msamiati katika lugha, hususan kwa dhana mpya zinazozuka kila uchao. Njia hizi hupendekeza jinsi wataalamu wanavyoweza kuunda msamiati mpya na kukidhidhi mawasiliano na kuziba pengo la kileksia. Njia hizi ni zifuatazo.

#### *Unyambuaji*

Unyambuaji ni njia mojawapo ya kuzalisha maneno katika lugha (O'Grady na wenzake, 1996; Fromkin na wenzake, 2007; Bauer, 1983). Hii ni njia ya kunyambua neno ili kuzaa neno lingine kusimamia dhana mpya au kuzaa neno jipya. Kwa mfano katika Kiswahili, neno *boresha* lilizaliwa kwa kunyambua kivumishi *bora, bidhaisha* (commoditization) kutoka nomino *bidhaa, rembesha* kutoka nomino *mrembo* n.k. Kwa hivyo Kiswahili kinaweza kutumia njia hii kuzalisha msamiati mpya kusimamia dhana mpya mbalimbali.

#### *Uzalishaji*

Uzalishaji wa maneno huletwa na uambishaji. Uambishaji ni kuongeza viambishi katika neno hususan kabla mzizi. Hii ni njia ya kimofolojia katika lugha. Mfano katika Kiingereza maneno kama, *undo, unearth, untread, unfit, ungodly, unhealthy, unhappy* n.k. yalitokana na kuweka kiambishi kabla ya mzizi wa neno (Fromkin na wenzake, 2007:89-91). Kwa hivyo katika kutafuta msamiati mpya katika Kiswahili, njia kama hii inaweza kusaidia kuzaa msamiati mpya.

#### *Uambatishaji*

Hii ni hali ya vipashio huru viwili au zaidi kukaa pamoja ili kuunda dhana moja mpya. (*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, 1990:14) Njia hii hutumika katika Kiingereza na kuzaa msamiati mpya (O'Grady na wenzake, 1996:151; Yule, 1997:65). Katika Kiswahili njia hii ilitumika kuunda maneno kusimimamia dhana mpya mfano *askarigongo, mwanaharamu, mwanajeshi, mwanahewa* n.k. Kwa hivyo njia hii inaweza vile vile kutumika.

#### *Uundaji*

Hii ni njia ya kuunda neno tu ama kwa kukopa au neno lililopo kusimamia dhana mpya. Kiingereza kilizaa maneno kutoka lugha nyingine au yaliyopo, mfano maneno *cepstrum* na *cepstral* kutoka maneno yaliyopo *spectrum* na *spectral* (Fromkin na wenzake, 2007:92-93). Yule (1997:64) akatoa mifano ya maneno yaliyoundwa katika Kiingereza; *nylon, zipper* na *xerox*. Katika Kiswahili kwa mfano, maneno *unyanyapaa (stigma), tarakilishi (computer), runinga (television), tovuti (internet)* ni maneno yaliyoundwa na wataalamu wa Kiswahili mfano Sheikh Nabahan na Rocha Chimera kusimamia dhana mbalimbali. King'ei katika Ogechi na wenzake, (2008:223) ameonyesha baadhi ya maneno ya Kiswahili kutokana na uundaji; *nywila* (password), *kiranja* (prefect), *karabati* (repair).

#### *Ujenzi ghairi*

Ni uundaji wa neno ambao huenda kinyume na utaratibu wa kawaida (*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, 1990:8). Fromkin na wenzake (2007:94) wanadai ni uundaji wa neno kutokana na kutojua mofolojia ya lugha. Hutokana na kutoelewa utaratibu fulani wa mofolojia ya lugha, hivyo watu kuunda neno na likakubalika. Wakatoa mfano wa maneno *stoke, swindle, peddle* kuwa yalitokana na watu kudhani kuwa kiambishi –er katika maneno husimamia mtenda, hivyo kitendo ni kutoa kiambishi hicho.

#### *Akronimi*

Ufupishaji huzaa akronimi. Haya ni maneno yanayotokana na ufupishaji wa maneno yaani kuchukua herufi moja moja katika kila neno na kuunda neno jipya (Fromkin na wenzake, 2007:98), mfano U.S.A (United States of America), A.U (Africa Union) n.k. Katika Kiswahili neno *Ukimwi* ni akronimu inayotokana na ‘Ukosefu wa kinga *mwilini*’n.k.

#### *Uhulutishaji*

Ni uundaji wa maneno ambapo sehemu za maneno mawili huunganishwa, na sehemu nyingine kudondoshwa na kuunda neno moja (Fromkin na wenzake, 2007:97). Fromkin na wenzake wakatoa mifano ya Kiingereza, maneno; *smog* (smoke + fog), *urinalysis* (urine + analysis) n.k. Katika Kiswahili kuna maneno *chajio* (chakula cha jioni), *chamcha* (chakula cha mchana) (*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, 199:9).

### *Ukopaji*

Ni njia ya kupata msamiati kwa kuhamisha kipashio kutoka lugha moja na kuingizwa katika lugha nyingine (*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, 1990:9). Mbinu hii imetumika katika kuzalisha msamiati wa Kiswahili mfano *motokaa* (motorcar), *shokomzoba* (shock absorber), *hela* (hela-Kijarumani), *hospitali* (hospital), *shukurani* (shukran-Kiarabu), *pesa* (paisa-Kihindi) n.k.

### *Ukatizaji*

Ni mbinu ambapo neno hupunguzwa silabi na kuwa neno moja (Yule, 1997:66). Mfano katika Kiingereza ni *flu* kutokana na influenza, *phone* kutokana na telephone, *brakutokana* na brassiere. Katika Kiswahili, sijapata maneno yaliyoundwa kutokana na mbinu hii lakini yanapatikana katika sheng mfano *hosî* kutokana na hospitali, *moti* kutokana na motokaa, *konda* kutokana na kondakta n.k.

Hizi ni mbinu ambazo wataalamu wa Kiswahili wanaweza kuzitumia kuzaa msamiati wa Kiswahili kusimamia dhana au vyombo mbalimbali. Kwa hivyo swala la ukosefu wa msamiati halina mashiko. Lililobaki ni juhud, ari na jitihada kwa wazungumzaji wa Kiswahili.

## **HITIMISHO**

Ni dhahiri kuwa maendeleo ni zaidi ya pato la nchi kuongezeka (*Domestic Gross Product*). Pia ni bayana mashambani kunachangia maendeleo ya nchi kwa uzalishaji maji na si kilimo tu. Maendeleo lazima yalete mabadiliko katika maisha ya umma nchini, na mabadiliko yenewe yawe chanya. Kinyume na hivi, nchi bado haijaendelea hata kama asilimia ya uchumi wa nchi inakua. Jambo hili lilitokea huko India, Pakistan, Taiwan, na baada ya nchi hizi kugundua hali hiyo, ikabidi mikakati ya kiuchumi ibadilishwe ili maendeleo yapatikane katika nchi. Watu wa mashambani walihusishwa zaidi na kufunzwa stadi mbalimbali kwa kutumia lugha zao wanazozitumia (Todaro, 1992, Desai, 1982, Miller, 1988).

Kwa hivyo, ili malengo haya ya maendeleo yawafikie wengi nchini kote hapa Kenya, lazima umma mashambani ujumuishwe kwa kuyajua malengo yenewe na kupata stadi mbalimbali (Mfano malengo ya sasa, 2018 ya Rais Uhuru Kenyatta- The Agenda Four). Haya yatawezekana kwa kutumia lugha inayotumika kwa wote minghairi ya kiwango cha elimu walichonacho. Lugha iliyofikia kiwango hiki hapa Kenya ni Kiswahili. Tumeona jinsi Kiswahili kinatumika huko mashambani katika Kaunti za Kwale, Uasin Gishu na Machakos katika uzalishaji mali. Wengi wameeleza na kusitiza jambo hili hapa nchini Kenya wakiwemo Mwita (2001), Shitemi (2001), Chimeara (1998), na wengine. Lakini hadi leo, serikali haijatilia maanani mawazo na mapendekezo haya. Hata hivyo, Profesa Anyang' Nyong' alipokuwa Waziri wa Uchumi na Mipango, alitoa mwongozo wa "*Mikakati Ya Kufufua Uchumi ili kuzalisha Mali na Ajira nchini Kenya 2003-2007*" mwaka wa 2003, chini ya serikali ya NARC ikiongozwa na Rais Mstaafu Mh. Mwai Kibaki. Hii ni hatua mwafaka kwani lugha zote mbili za Kitaifa zilitumika Kiingereza na Kiswahili. Na katika mwaka wa 2010 *Katiba Mpya ya Kenya* iliandikwa kwa lugha zote mbili rasmi, Kiswahili na Kingereza. Jambo hili lilifanya umma kufahamu haki zao zaidi na sera za

serikali katika ugavi wa mali mashinani chini ya mfumo wa ugatuvi. King'ei (2008) ametoa mifano ya istilahi za Kiswahili katika teknolojia ya Habari na Mawasiliano anbazoziliuundwa au kokopwa na zinatumika. Hili ni dhihirisho kuwa tunapoanza jambo, basi istilahi zitapatikana kwa sababu ya hiyo haja. Ikumbukwe, “*necessity is the mother of invention*”.

Kwa hivyo, ili maendeleo yapatikane mashambani, lugha ya Kiswahili izidi kutumika kusambaza sera za serikali na kufunza jamii za mashambani stadi mbalimbali, mifano mbinu bora za kilimo na ufugaji, uhunzi, uashi n.k. Hii itasaidia uzalishaji mali zaidi na matokeo ni maendeleo ya jumla kuchipuka. Aidha maisha ya jamii kuwa bora zaidi.

## MAREJELEO

- Bauer, Laurie (1983) *English Word-Formation*, Cambridge: C.U.P
- Chimera, Rocha (1998) *KISWAHILI: Past, Present and Future Horizons*, Nairobi: Nairobi University Press
- Daily Nation*, 12<sup>th</sup> June 2014 “The Budget” kurasa 4-8
- Desai, S.S.M (1982) *Economic History of India*, New Delhi: Himalaya Publishing House
- Fromkin Victoria na wenzake (2007) *An Introduction to Language*, Wadsworth: Thomson Ltd
- King'ei, Geoffrey K (2008) “Masuala ya Kinadharia katika ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili: Mifano kutokana na mradi wa Kamusi wa Microsoft” katika Ogechi, Nathan O. na wenzake, *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*, Eldoret: Moi University Press, uk 221-226.
- Miller Rodger Leroy (1988) *Economics*, New York: Scibner Educational Publisher
- Murdoch, William M (1980) *The Poverty of Nations: The Political Economy of Hunger and Population*, Maryland: Johns Hopkins University Press
- Mwita, B. Mariam (2001) “Language a Creative Force and a Fundamental Tool for Civilization and Development” ktk Shitemi N. na Noordin M (wahariri) *Kiswahili: A Tool for Development*, Eldoret: Moi University Press, kurasa 124-131
- O’Grady na wenzake (1996) *Contemporary Linguistics: An Introduction*, Harlow: Longman
- Rashidi, Linda Stump (1992) “Towards an Understanding of the notion of Theme: an example from Dari” ktk Davies Martin na Ravelli, Lousine (wahariri) *Advances in Systemic Linguistics*, London: Printer Publishers Ltd, kurasa 123-146
- Rono, Phillip K. (2001) “Communication of New Ideas and Innovations: The Role of Language Agents and Change Agents in Rural Development” katika Shitemi, N na Noordin, M (wahariri) *Kiswahili: A Tool for Development*, Eldoret: Moi University Press, kurasa 133-140
- Roodney, Walter (1989) *How Europe Underdeveloped Africa*, Nairobi: East Africa Educational Publishers
- Shitemi, Naomi L (2001) “Language as a Tool for Development: Issues to Ponder” ktk Shitemi, N na Noordin, M (2001) *Kiswahili: A Tool for Development*, Eldoret: Moi University Press
- The Standard Newspapaer*, 12<sup>th</sup> June 2014 “The Budget”
- The World Bank, Washington (2009) *Directions in Development: Human Development; Accelerating Catch-Up*
- Todaro, P. Michael (1992) *Economics for a Developing World*, New York: Longman

Publisher

Yule George (1997) *The Study of Language*, Cambridge: Cambridge University Press